
REPUBLIC OF KENYA
THE COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA

OFFICIAL REPORT

Wednesday, 18th April, 2018

The House met at 2:35p.m.

(The Temporary Speaker (Hon. Raphael Bwire) in the Chair)

PRAYERS

The Temporary Speaker: You may be seated Members, once again welcome back to our plenary ready for today's business. Mr. Clerk?

MOTION

ENHANCEMENT OF PRE-PRIMARY EDUCATION IN MOMBASA COUNTY

Hon. Charles Kitula.

Chief Whip (Hon. Kitula):

(Chief Whip (Hon. Kitula) moved the Motion)

THAT AWARE that part 2 (2) of the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya, 2010 mandates the County government to take the charge of pre-primary education, village polytechnics, home craft centers and children facilities;

FURTHER AWARE that pre-primary education forms the basic foundation of the entire education system;

NOTING THAT many public pre - primary education centers in the County are in critical conditions and lack basic learning equipment;

CONCERNED THAT lack of immediate response might jeopardize early childhood education in the County;

I therefore urge this Assembly to RESOLVE that the County government of Mombasa through the Department of Education to;

1. Incorporate donors and well-wishers in building/renovating all public pre-primary education centres in the County;
2. Provide learning equipment to all public pre-primary centers;
3. Give first priority during employment to teachers currently working at various pre-primary education centers in the County.

Thank you Mr. Speaker sir may I ask Hon. Ogotu to second my Motion.

Hon. Ogotu: Thank you Mr. Speaker I second.

(Question proposed)

The Temporary Speaker: Hon. Members I now propose the question, the Motion moved by Hon. Charles Kitula on enhancement of pre-primary education in Mombasa County be considered by this Hon. House in the same terms as moved?

(Question proposed and agreed to)

Yes the Motion mover.

Chief Whip (Hon. Kitula): Ahsante sana Mheshimiwa Spika, ningependa pia vile vile kuweza kushukuru Bunge hili kutoa ruhusa ili tuweze kuchangia mada ya leo na kusema ukweli ningependa kuwahimiza wenzangu ili tuweze kushirikiana kuweza kuhakikisha ya kwamba hoja hii imeweza kupita kwa Bunge hili maana elimu ya chekechea hivi sasa katika serikali ya Kaunti yetu ya Mombasa inaenda kuzorota.

Kusema kweli serikali imeweza kuunda chuo cha kisasa cha chekechea Likoni na vile vile Jomvu na hivi sasa eneo la Bunge la Nyali lakini hivi sasa katika shule za serikali kila shule ya serikali ina shule ya chekechea ndio maana lengo letu kuu siku ya leo ningependa kuwahimiza Bunge hili kwamba tupatie ruhusa ya idara ya elimu iweze kutafuta wafadhili ili zile shule za serikali pia nazo ziweze kupatiwa ya ufadhili ya kuweza kukarabatiwa kwa njia ya kisasa na muundo wa kileo.

Vile vile ningependa pia kuwahimiza idara hii ya elimu iweze kuhakikisha kwamba shule hizi pia zina stakabadhi na vifaa kutoa elimu bora kwa watoto wetu wa chekechea, vilevile Mheshimiwa Spika kuna tetesi sana kati ya sisi viongozi na waajiriwa ambao wameweza kuajiriwa hivi karibuni katika shule za chekechea ikiwa mashinani watu wameajiriwa ni watu ambao hawana ufahamu zaidi kuhusu jinsi gani walioweza kuleta watoto wao wa chekechea katika shule hizi na vile vile kuna tetesi ya kwamba wengi wameweza kuajiriwa lakini hawana ufahamu zaidi kuhusu masuala haya ya chekechea.

Waweza pata mwalimu amesema kitengo cha kufunza shule kuu lakini kwa sababu ya ukosefu wa kazi wameweza kuchukua kazi hizi za ualimu wa chekechea ndio maana nahimiza Wabunge wenzangu tuweze kuwapatia kipao mbele wale walimu ambao hivi sasa wanafunza katika shule hizi wakati wa kuajiriwa waweze kuajiriwa kwa mapema na nafasi za kwanza waweze kupatiwa hao ambao wako kwa sehemu hizi maana hao ndio wanajua changamoto kuu na wanajua jinsi gani watoto wao wanapitia maana hatari walioweza kubarikiwa kipaji cha kuweza kutunza watoto wangali wanakua.

Mheshimiwa Spika ningependa sana Wabunge wenzangu waweze kuchangia hoja hii na kuweza kuhakikisha kwamba tunapitisha ili tuweze kuwapatia motisha wananchi mashinani na watoto waweze kupata elimu bora ya chekechea, ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker: Thank you Hon. Member now Hon. Members the floor is open for insight, yes Hon. Amur.

Hon. Amur: Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika hoja ilioletwa mbele yetu ni hoja ya maana lakini twende mbele ama turudi nyuma Mheshimiwa Mohamed Hatimy alileta Mswada ndani ya Bunge hili kwamba ni muhimu kwamba sisi tuwe na *data* bila kuwa na *data* ya wale vijana ama hizi shule tutakuwa tunaimba kama kasuku. Mheshimiwa Spika ni lazima tuwe na *data* tujue shule zenyewe ni ngapi, wanafunzi ni wangapi, Walimu ni wangapi? Kutoka hapo mfumo bora utapatikana, aidha ya hio ikiwa tutakuwa takirishi maalumu za kufahamisha kwamba walimu ni wangapi, shule zenyewe ni ngapi? Wanafunzi ni wangapi.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika lile tulilozungumza juzi kwamba ni lazima kuwe na *data* ili tuweze kujua watu wote ni wangapi, wanafunzi ni wangapi? Walimu ni wangapi, hapo tutapata muongozo Mheshimiwa Spika. Mswada wenyewe ni mzuri lakini unataka utiliwe mkazo ili tupate takirishi kamili za kutueleza kwamba shule ni ngapi, walimu walioajiriwa ni wangapi na ikiwa kuna walimu walio ajiriwa hawana ufahamu basi kosa hili lichukuliwe kwa wale walio ajiri watu wale kwa sababu huwezi kuchukua walimu wa shule za msingi ukaenda ukawapeleka kwa chekechea, ikiwa kuna ushahidi wa kutosha ni jukumu letu sisi kuchukua stakabadhi hizi na tuwafuate wanaohusika tuone kwamba wale walionyimwa nafasi zile ambao wenye ujuzi si haki hata kidogo. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker: Thank you Hon. Murfad. Yes Hon. Hatimy?

Hon. Mohamed Hatimy: Mheshimiwa Spika mimi sina shida na huu Mswada isipokuwa tunajua vizuri sana kuwa sehemu ya nne ya Katiba inagawanya majukumu ya Kaunti na serikali kuu. Mheshimiwa Spika itakuwa vigumu sisi kuinua kwenye shule za msingi kwa sababu ni jukumu la serikali kuu, kwa hivyo ilikuwa naomba *mover* wa huu Mswada kama twaweza pamoja na Kamati ya elimu tupeane mawazo ujaribu kuirekebisha hii...

(Interruption)

The Temporary Speaker: What is your point of information Hon. Ogutu?

Hon. Ogutu: I think number two is public pre primary education and that within our mandate.

The Temporary Speaker: Are you well informed Hon. Hatimy?

Hon. Mohamed Hatimy: Mheshimiwa Spika labda atueleze amemaanisha jambo gani *pre primary* kwa sababu shule zimegawanywa; kuna kipande kiko kwa Kaunti, kuna vipande viko kwa serikali kuu tuna anuai ziko kwa Kaunti, kuna vyuo vikuu serikali kuu. Sasa labda atueleze amemaanisha kitu gani Mheshimiwa Spika kwa sababu sisi kama Kaunti hatuwezi kwa mfano kutoa pesa zetu za Kaunti kwenda kutengeza shule ambazo ni za serikali kuu nafikiri itakuwa kinyume cha sheria, itabidi lazima twende kwa *intergovernmental* ambayo inasimamiwa na Naibu wa Raisi Mheshimiwa Ruto wakubali lile jukumu watuletee sisi alafu sisi ndio tufanye sasa sijui amemaanisha kitu gani *pre primary*.

The Temporary Speaker: Thank you Hon. Hatimy, the Motion mover Hon. Kitula I think you will clarify what you meant in your Motion; is it the ECD that are under the mandate of the County government or the pre - primary school? What do you mean with specifically pre-primary school?

(Silence)

Do we have teachers in the House?

Hon. Amur: Mr. Speaker with all due respect pre to me is referring to ECDS as per Schedule Four, thank you.

The Temporary Speaker: Thank you Hon. Amur, the Motion mover as you peruse your Constitution did you specifically mean the ECDs or you meant something else?

Chief Whip (Hon. Kitula): Ahsante Mheshimiwa Spika, *pre- primary school* kulingana na maana yake ni kuweza kusoma kulingana na Kamusi inasema hivi, *a pre-school also known as nursery school, pre-school or kindergarten is an educational establishment or learning space offering early childhood education.* That is ECD Mr. Speaker.

The Temporary Speaker: Thank you for the clarification. I think Hon. Hatimy, i think you captured what the Motion mover clarified, the pre-primary centers simply means according to his dictionary the ECDs and kindergartens are those under the mandate of the County government, if am not wrong. So I think we will contribute from there; we wanted the clarification whether you were meaning the primary schools that are under the central government or the pre-primary, you have clarified i am now informing the Member who raised the concern. So I think we will take it from there Hon. Hatimy now that it has been clarified by the dictionary.

Hon. Mohamed Hatimy: He can do a research and come and tell us what it means or maybe the Clerk can give us an insight.

The Temporary Speaker: I think the Clerk is also seconding the clarification from the Motion mover that it simply means the ECD, yes.

Hon. Mohamed Hatimy: Mheshimiwa Spika kama ni ECD, juzi tumefanya *public participation* ya CIDP na kuwa maoni ya watu tuangalie kwenye CIDP watakuwa wamesema nini, ama itabidi ije kwenye mipangilio kwa sababu hapa tunazungumzia pesa nyingi sana na hivi vitu ambavyo tunavizungumzia, sijui kama *mover* ameweza kwa sababu hapa tunazungumzia pesa nyingi sana hivi vitu ambavyo tunavizungumzia. Kwa hivyo sijui kama muendeshaji Hoja ameweza ku...

(Interruption)

Hon. Ogutu: Point of information again.

The Temporary Speaker: Order! Order Hon. Member...

(Interruption)

Hon. Mohamed Hatimy: I think I don't want to be informed Hon. Speaker.

The Temporary Speaker: Okay! The Members... Order! But Mr. I mean Hon. Hatimy

Hon. Mohamed Hatimy: Mmmhh... (Nodded).

The Temporary Speaker: I think, I don't know whether it's my eyes or something the Motion mover asked the House to resolve that we incorporate the donors and well-wishers in building and renovating all these public pre-primary education centers. So this is simple out of our budget!

Hon. Mohamed Hatimy: So this is simple out of our budget?

The Temporary Speaker: Yes.

Hon. Mohamed Hatimy: Then I support Hon. Speaker.

The Temporary Speaker: Thank you.

(Applause)

Yes Hon. Ramla?

Hon. (Ms.) Ramla Said: I am supporting the Motion. It is a good one; I am only insisting on while innovating we should always think of children with disability. We should help them in the school, we should help teachers who are trained in the special needs so I support the Motion but I also insist on thinking of people with disability. Thank you.

The Temporary Speaker: Thank you Hon. Member next time Hon. Kitula you capture the people living with disability that is the concern. Hon. Osongo, you had a concern?

Hon. (Ms.) Osongo: Thank you Mr. Speaker. I had a concern about the pre-primary as the schedule that is given out this time. The pre-primary is from class three coming down because I see even my child is in class two and it is being written pre-primary, so the system is changing...

(Interruption)

The Temporary Speaker: Hon. Member! Hon. Members we have just been clarified and I think we will strictly conduct our Business under the clarification that have been given. Yes please! Yes Hon.? Renson you will wait just a minute.

(Consultations)

Hon. Thoya: Thank you Mr. Speaker I want to take this opportunity to appreciate Hon. Kitula for coming up with this very noble Motion, I beg to support and say that we need to use all our resources available in this County to ensure that we get it right because we understand early childhood education is the basic foundation for greater heights of education so if we get it right from the nursery school it is our belief that going to Primary, Secondary and University is going to be very easy. Apart from maybe supporting I am getting it very nice at point number 3 as we are going to pass this Motion we want put it black and white the issue of employment of teachers that in the near future they need to get it right especially those people that have been volunteering for period of years to be given that opportunity and same to the department of Education.

I think earlier on I had a meeting on the issue of these teachers that have been volunteering in ECD and when recruitment comes on their way they do not get that opportunity. So it is a great opportunity that we are getting here that as we pass a follow up on the same must be done that these teachers that have been volunteering in the ECD must be considered. Thank you.

The Temporary Speaker: Thank you Hon. Member. Hon. Hamida?

Hon. (Ms.) Sheikh Ali: Thank you Mr. Speaker sir, I want to add on by saying that we need more ECDs on all Sub Counties because there are over flooded with so many children in one place and more teachers as my fellow colleague has just said and I think we need to train even more teachers for the ECDs if we take them in as well and to have more students in our places. Thank you.

The Temporary Speaker: Hon. Athuman?

Hon. Shebe Athuman Salim: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii kuweza kuchangia Mjadala huu, ningependa kuunga mkono kwanza Mheshimiwa mwenzangu Kitula kuja na huu Mswada ila napenda tu kutilia mkazo pointi namba tatu ambayo Mheshimiwa ameweza kuiweka hapa kwa sababu tukiangalia Jomvu kumefanyika kazi kubwa sana hususan katika masuala mazima ya elimu ya chekechea. Kama kuna shule imejengwa watu waweza kuiga basi nafikiri mfano wa kuigwa ni wa Jomvu, kwa hivyo nampongeza na namshukuru Gavana kuangalia eneo langu Jomvu na kuweka madarasa ya kisasa ya ECD.

Changamoto tu Mheshimiwa Spika ni na hii niliileta ni kawi na Mwenyekiti wa Elimu Mheshimiwa Bomoa (Ibrahim Omondi) zile nafasi ambazo wanaofundisha pale walimu unakuta wengine si wa kutoka katika yale maeneo na wengine pia fani ile ya chekechea bado hawajaboea ina maana wanafundisha shule za msingi.

Kwa hivyo ni aula ningependa vizuri hili Bunge tuweze kuchukua utaratibu muafaka tuangalie hizi shule za chekechea walimu ni wangapi, wanatoka wapi na je wasomea fani hiyo ukweli ama ni wengine wanatolewa katika sehemu zengine ama wanatolewa katika nyanja nyengine kuweza kusomesha. Mimi ningependelea tutilie mkono sana masuala hayo Mheshimiwa Spika. Ahsante sana.

The Temporary Speaker: Thank you. Hon. Naliaka.

Hon. (Ms.) Wafula: Ahsante Bwana Spika kwa kunipa nafasi hii, mimi ningependa kumpongeza aliyeleta huu mjadala Bwana Kitula. Kwa kweli Mswahili anasema, *samaki mkunje angali mbichi* na mtoto asipoelewa hata mambo ya hati akiwa katika shule ya chekechea mara nyingi utapata hata kuandika kwake kunakua ni shida na nyumba hata ukaijenga vizuri vipi ikiwa haina msingi bora itafika juu na utapata mara nyingi inabomoka. Kwa hivyo ningependa tu kuongeza sauti yangu ya kwamba tuheshimu hicho kitengo cha chekechea na tuweze kukipa kipao mbele cha kwanza cha kuweza kuziwezesha tuzipe nguvu ili kwamba watoto wetu waweze kutoka chini wakiwa na msingi bora wa ki elimu.

Jambo lingine ningependa kusema hivi huwezi tuma mtu kulima na hujapewa jembe, kwa hivyo hawa walimu kusema hakika itabidi tuwapatie vifaa vile ambavyo kwa kimombo wanasema *teaching aids* ambazo wawe nazo za kusaidia hawa watoto ili waweze kuelewa kwa haraka na yale madarasa vile wenzangu wametangulia kusema tuweze kuyafanikisha yaweze kuchukua idadi ambayo itafaa kwa mwalimu ili iwe pia kazi rahisi kwa mwalimu kuweza kuwasaidia watoto wetu. Kwa hayo machache ahsante sana Bwana Spika.

The Temporary Speaker: Hon. Milka?

Hon. (Ms.) Ngare: Thank you Mr. Speaker. This being my area of expertise I would like to contribute something; I want to start by congratulating the mover of the Motion Hon. Kitula for taking into consideration the pre primary education for our children. And just to add my voice to what the other Hon. Members have stated pre primary education is just a another way of talking of ECD schools specifically Kg 1, Kg 2 and Kg 3 nothing to do with Std 1, 2 and 3, so let the Hon. Members who think so be informed.

Having a proper foundation for a child in school is key to the child's learning in later stages of life, education to begin with is key to development in many areas, when a child goes through a proper system in pre primary education that child grasps or the fact they are going to learn in the later years is smooth and they do not encounter any challenges. It is just like building a house on quick sand, we build a house on quick sand and you do not put the proper foundation that house is easily going to collapse.

Now laying a strong foundation for a child is therefore key and the mover of the Motion has stated it is true, these children should get a conducive learning atmosphere and there should be proper equipments like building and learning resources and of course the teachers need to have training so they know how to handle the children. And of course they should be motivated and the class numbers should be manageable so that our children are able to gain maximally from the teachers, having also a class of 100 like is the case in Mombasa right now, 100 pupils per teacher is quite challenging and they would not be able to achieve much.

As the Motion stands I want to support it 100 per cent and to ask our fellow Hon. Members to also support if the standards of learning in this County are to improve and our children to be shining stars in future. Thank you, Mr. Speaker.

The Temporary Speaker: Thank you. Yes Hon. Feddis Mbura.

Hon. (Ms.) Mbura: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa nafasi hii, kwanza nampongeza Mheshimiwa mwenzangu kwa kuleta Mswada huu. Mimi nauunga mkono asilimia 99 kwa sababu kwangu tayari kuna ule umbali wa shule.

Kwangu Mwakirunge kwa upande huu wa kwamba tutafute wafadhili ili tuweze kurekebisha zile shule mimi naunga mkono na Mheshimiwa Gavana anayo nafasi kubwa sana ya kupata wafadhili. Kwa hivyo mimi ningeomba hii pointi namba moja Mheshimiwa Gavana aweze kutafuta wafadhili ili zile shule ambazo ziko kule mashinani zikaweze kurekebishwa na watoto waweze kuendelea vizuri na pointi namba mbili pia kuhusu kuleta vifaa pia ningeomba hivi vifaa viweze kuletwa katika mashule ili watoto kulingana na huu mbadiliko wa elimu waweze kupata elimu kulingana na vile inavyotakikana na pointi namba tatu ya kwamba wapewe vipao mbele walimu wa kule mashinani.

Hili jambo mimi naliunga mkono mia fil mia wacha tisaini na tisa kwa sababu ya kwamba mwalimu akitolewa nje ya ile Wodi akifika pale hamalizi hata wiki mbili tatu anajiuzulu na anatoka kwa sababu ya yale ya maisha ya kule kwetu. Kwa hivyo mimi naunga mkono mia kwa mia wale walimu wachukuliwe kwa lile eneo kwa sababu wao wamezoea mazingira ya pale, wamezoea kila jambo la pale mtaani ama pale kijijini kwake. Hivyo basi mimi naunga mkono na hili nalipa kipao mbele wakati walimu wanapoteuliwa wateuliwe walimu wa ile ile sehemu ambayo wametoka ili waweze kuwa na ufundisho mzuri ama waweze kuendeleza kazi zao katika hali ambayo ni ya uzoefu. Ahsante sana Bwana Spika na Mungu amuweke Bwana Kitula.

The Temporary Speaker: Thank you, yes Hon. Shomari.

Hon. Ali Mohamed Shomari: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezeshwa kukutana sote hapa. Pili natoa shukrani za dhati ningependa kumpongeza Bwana Kitula, tatu ningependa kueleza Bunge hili kwamba lituangelie kwa jicho la huruma wana Magogoni kwa sababu upande wa elimu naona Kaunti yetu ya Mombasa imetusahau kabisa hatuna hata hiyo shule za chekechea (ECD), hata shule ya msingi (Primary), hatuna mradi wowote serikali ya Kaunti imefanya katika Wodi yetu ya Magogoni. Kwa hivyo naomba kitengo cha elimu kiangelie kwa makini eneo la Magogoni sisi tupate hata kama ni ECD moja. Tunapongeza Mswada kama huu wa elimu angalau pia Magogoni iwe tumesaidika. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

(Applause)

The Temporary Speaker: That is a concern raised, thank you Hon. Member. Yes Hon. Leila Nyache.

Hon. (Mrs.) Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia, kwanza nampongeza Mheshimiwa mwenzetu Mheshimiwa Kitula kwa kutuletea hoja hii ya maana sana ya shule za chekechea. Mheshimiwa Spika mimi ningependa kuongea juu ya mazingira ya hizi shule za chekechea, wanafunzi wetu watapewa vifaa vya kusomea, watapewa walimu lakini mazingira yakiwa mabaya pia elimu nayo haitaingia akilini.

Kwa hivyo mimi nasema kupitia shule yangu ya Msingi ya Kwa Hola kuna shule ya chekechea pale watoto wanasoma ndani ya shule ya mabamba, shule yote kuanzia juu mpaka chini imejengwa na mabamba Mheshimiwa Spika. Kwa hivyo ningeomba huu ukarabati unaoendelea ama huo urekebishaji unaoendelea kwa hizi shule za chekechea uanze kufanywa kwa haraka kwa sababu wale watoto wakati wa joto huwa wanatolewa chini ya muembe wakisomea nje chini ya muembe kwa sababu ya joto limezidi na saa hizi mvua imenyeshwa watoto wameingiwa na baridi.

Hivyo basi mimi ningeomba hiyo shule ya chekechea ya Kwa Hola Primary iweze kuangaliwa sana kwa kina na kama ni masuala ya urekebishaji ama ujenzi iwe kipao mbele kujengwa manake watoto wetu wanaumia sana. Ahsante sana Bwana Spika.

(Applause)

The Temporary Speaker: Thank you, Hon. Ogutu.

Hon. Ogutu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika nafikiri mengi yameongelewa, mimi wasiwasi wangu iko katika maombi nambari moja. Nafikiri Mheshimiwa Spika ili wafadhili waweze kujenga hizi shule zetu lazima twende kasi ya ziada ya kuhakikisha kwamba hizi shule zetu za umma zimepata hati miliki, nyingi ya hizi shule hazina hati miliki. Hivyo basi nafikiri idara husika inatakikana tuhakikishe kwamba shule zetu zimepata hizo hati miliki. Ahsante sana.

(Applause)

The Temporary Speaker: Yes Hon. Members you seem to have exhausted your deliberations I will now call upon the Motion Mover to respond.

Chief Whip (Hon. Kitula): Ahsante Mheshimiwa Spika, mimi ninashukuru Wabunge wenzangu na kusema kweli janga la elimu ya chekechea ni msingi wa elimu yeyote katika nchi yeyote ya Kenya na mimi ningependa kutoa shukrani hasa kwa kila mmoja aliyeweza kuchangia. Ama kwa kweli iliobakia zaidi ni mimi kama mmoja wa wanakamati wa Kamati hii ya elimu tutilie mkazo kuhakikisha kwamba hoja hii imeweza kufika mahali ambapo mimi kama ni mwenye kuileta hoja hii niweze kuhakikisha kwamba imeweza kutimizika katika sehemu zetu za uwakilishi. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker: Thank you, before now I put the question it must be captured that the issue of employment was also raised within the Motion and we also pray that it is captured that the experienced teachers are very competent one; in fact to be considered first and the locals to avoid confrontations with other people. Hon. Members now allow me to put a question. I now put a question that enhancement of Pre-Primary Education Mombasa County be considered by this Honorable House in the same terms as moved.

(Question put and agreed to)

...Next order?

ADJOURNMENT

The House stands adjourned until Thursday 19th April, 2018 at 2:30p.m.

The House rose at 3:12p.m.